


Jinsi Viumbe wa Roho Wanavyohusika Maishani Mwetu (Sehemu ya 2)

Inategemea sura ya 10 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye jw.org/sw.

LENGO: Chunguza yale unayoamini na sababu inayokufanya uamini hivyo, chunguza yale ambayo Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine yale unayoamini.



JE, NI VIBAYA KUWASILIANA NA PEPO?

1 CHUNGUZA YALE UNAYOAMINI

Kwa nini huenda wengine wakasema hapana?

Kwa nini huenda wengine wakasema ndiyo?

Wewe unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?

2

CHUNGUZA YALE AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA

Neno la Mungu linakataza zoea la kuwasiliana na pepo, njia inayotumiwa na roho waovu kuwapotosha watu.
(Ona sura ya 10 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 9-13.)

Soma Kumbukumbu la Torati 18:10, 11 na Wagalatia 5:19-21.

Mistari hiyo inaonyeshaje maoni ya Yehova kuhusu kuwasiliana na pepo?

Soma Ufunuo 12:12, 17.

Kwa nini Shetani na roho wake waovu wana lengo la kuendelea kuwapotosha watu?



Ikiwa huwezi kumkaribisha mhalifu nyumbani kwako, basi pia, usiwakaribishe roho waovu katika maisha yako.

Yehova atatusaidia kuwapinga roho waovu.

(Ona sura ya 10 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 14-19.)

Soma Matendo 19:19.

Kulingana na simulizi hilo lililoongozwa na roho, Wakristo wa karne ya kwanza huko Efeso waliweka kielelezo gani kizuri cha kupinga zoea la kuwasiliana na roho?

Soma Methali 18:10; Waefeso 6:16; na Yakobo 4:7, 8.

Ni maandalizi gani kutoka kwa Yehova yanayotusaidia kumpinga Shetani na roho wake waovu?

Kwa nini unathamini kujua kwamba Yehova ana nguvu nyingi kuliko roho waovu na anataka kutusaidia?

3

ELEZA YALE UNAYOAMINI

IKIWA MTU ANASEMA...

Si vibaya kubashiri kwa kuwa ni burudani isiyo na madhara.

UNAWENZA KUMWAMBIA...

Watu wengi wana maoni kama hayo. Lakini mimi siamini hivyo kwa sababu...

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?

IKIWA MTU ANASEMA...

Roho waovu wana nguvu sana, hivyo hatuwezi kuwapinga.

UNAWENZA KUMWAMBIA...

Ni kweli kwamba roho waovu wana nguvu sana. Lakini naamini kwamba *tunaweza* kuwapinga kwa sababu...

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?
